

**WIZARA YA AFYA**

**MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA**



**UPOKEAJI WA MALALAMIKO YA WATUMIAJI WA CHAKULA**

**UTANGULIZI**

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) pamoja na majukumu mengine yaliyoanishwa kwenye sheria, ina jukumu la kupokea na kushughulikia malalamiko yanayotokana na vyakula ambavyo havifai kwa matumizi au mwenendo ambao katika uzalishaji, uhifadhi, ugawaji au uuzaji unaoashiria kuwepo kwa vyakula ambavyo havifai kwa matumizi ya binadamu.

Ili kufanikisha jukumu hilo muhimu, TFDA hupokea taarifa hizo kutoka kwa Wadau na hasa walaji vyakula. Taifa hizo hutumiwa na TFDA katika kuchukua hatua zinazostahili kulinda afya ya walaji wa vyakula. Mamlaka inazingatia wajibu wake wa kisheria wa kutunza siri na majina ya watu wanaotoa taarifa hizo inapokuwa ni lazima kufanya hivyo.

**UTARATIBU WA KUPOKEA MALALAMIKO YA WALAJI WA VYAKULA**

1. Peleka malalamiko yako katika Ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa zilizopo karibu na EPI – Mabibo External au unaweza kwenda kwenye ofisi yoyote ya afya katika Halmashauri iliyo karibu nawe na kutoa malalamiko yako.
2. Wasilisha malalamiko yako kwa maandishi ya kwa mdomo n.k. kuhusu vyakula vibovu kwa **Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Chakula na Dawa, au kwa Afisa Afya Mfawidhi** wa Halmashauri husika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:
  - Jina, anuani pamoja na namba ya simu yako. Msingi wa malalamiko husika, eneo na wakati wa tukio, idadi ya waathirika, hatua zilizochukulia baada ya tukio n.k Aina ya chakula au vyakula vinavyolalalmikiwa

- Uthibitisho (kama upo) wa madhara yoyote ya kiafya kutokana na matumizi ya chakula hicho/husika
- Anuani ya hospitali/kituo cha afya au majina ya madaktari waliohusika kuwa hudumia waathirika
- Mabaki ya chakula kinacholalamikiwa yatumwe/yapelekwe TFDA na ikiwezekana yawe katika makasha ambayo hayajafunguliwa ili kuepusha uchafuzi au dosari za uchukuaji wa sampuli zinazoweza kujitokeza.

Mamlaka inawakaribisha watu kutoa taarifa sahihi ambazo zitasaidia kuboresha lengo zima la kuwalinda walaji dhidi ya athari mbalimbali za vyakula visivyofaa.

**IMETOLEWA NA:**

**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)**  
**S.L.P. 77150**  
**Dar es Salaam**  
**Simu: 255 – 22 2450512/2450751/2452108**  
**Fax: 255 – 22 2450793**  
**E-mail: [tfda @ simbanet.net](mailto:tfda@simbanet.net)**  
**Tovuti: [www.tfda.or.tz](http://www.tfda.or.tz)**